

Maswali

1. Wana mapacha wa Isaka na Rebeka waliitwa nani?
2. Pacha yupi alizaliwa kwanza?
3. Haki ya urithi wa mzaliwa wa kwanza ulikuwa nini?
4. Mungu alisema ni mwana yupi atapata baraka?
5. Esau alibadilisha nini na haki yake ya kuzaliwa?
6. Isaka alitaka Esau afanye nini?
7. Isaka alisema atapea Esau nini?
8. Rebeka na Yakobo walifanya nini ili wamdanganye Isaka?
9. Nani alipata baraka?
10. Uongo ulizababisha huzuni gani?

Majibu

1. Esau na Yakobo.
2. Esau.
3. Alipata baraka na ahadi za Mungu.
4. Mungu alisema kwamba mwana mdogo, Yakobo, ndiye atapata baraka.
5. Esau alibadilisha haki ya mzaliwa wa kwanza na bakuli ya kitoweo.
6. Isaka alimwambia Esau aende kuwinda swara ili amtengenezee chakula cha mwituni.
7. Isaka alisema atampa Esau baraka.
8. Rebeka alimvalisha Yakobo nguo za Esau na kumwekea ngozi za mbuzi. Yakobo alijifanya kuwa Esau na akamdanganya babake.
9. Yakobo alipata baraka.
10. Esau alimchukia Yakobo. Yakobo alienda nchi ya mbali na hakumwona mamaye Rebeka kwa mda mrefu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1



8 Yakobo na Esau

Kwa Biblia Mwanzo 25:19 – 34 na mlango 37

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba ahadi za Mungu ni za muhimu katika maisha yetu.

Somo

Baada ya Isaka na Rebeka kuoana kwa miaka mingi, Rebeka alipata wana mapacha. Waliitwa Esau na Yakobo. Hawa mapacha walikua wakiwa tofauti sana.

Esau alikuwa mtu mwekundu na malaika mwilini. Alikua akiwa mwenye kuwinda. Alipenda na kufurahia kuwinda, kufukuza na kukimbia. Alipenda kuishi kwa vilima na vichakani. Alifurahia kutafuta hali akiwinda. Esau aliletea familia nyama mzuri ya swara, ngurwe ya mstuni, ndege na samaki.

Yakobo alipenda nyumbani kwao. Alikuwa mkulima. Alichunga mifugo ya baba yake. Na labda alilima akipanda ngano na sayari. Isaka alipenda Esau aliyemwindia nyama alizopenda – nyama ya mwituni. Rebeka alimpenda Yakobo.

Mungu alimpa Ibrahimu ahadi na baraka za kipekee. Hizi baraka zilipokezwa kwa kila mzaliwa wa kwanza wa familia. Kila mwana mkubwa wa huo ukoo alikuwa mrithi wa hizo baraka na ahadi za Mungu. Hizi zilikuwa **haki za kuzaliwa**. Baraka zilikuwa **haki** za mwana mkubwa kwa sababu ya **kuzaliwa** kama wa kwanza kwa familia.

Kwa hivyo Ibrahimu alimpa mwanawe wa kwanza Isaka. Isaka alipata mapacha, na Esau alizaliwa kwanza. Anasitahili apate baraka za mzaliwa wa kwanza. Lakini kabla ya mapacha kuzaliwa Mungu alimwambia Rebeka kwamba mdogo atakuwa wa hizo baraka. Yakobo alikuwa pacha mdogo.

Siku moja Esau alikuja nyumbani kutoka mawindoni. Hakukuwa amekula chakula kwa mda. Alikuwa na njaa sana. Yakobo alikuwa anatengeneza kitoweo kizuri. Esau alimwomba amsaidie hicho kitoweo. Yakobo alikuwa ametaka baraka za Mungu kuliko kitu kingine chochote. Yakobo alimwambia Isaka kwamba atampa chakula kwa kumuuzia baraka za mzaliwa wa kwanza ikiwa atambadishia. Esau alivutwa na mnuko wa chakula kilichokuwa kikitokota mekoni. Alikuwa na njaa sana na hakujali maneno ya haki za mzaliwa. Alikubali Yakobo achukue haki za kuzaliwa. Alikaa na akala hicho kitoweo. Kwa hivyo Esau akauza haki zake za baraka na ahadi kutoka kwa Mungu kwa ajili ya chakula.

Baada ya miaka mingi Isaka alikuwa mgonjwa na macho hayakuona vizuri. Isaka alitamani kula nyama ya mwituni iliyoletwa na Esau. Isaka alimwita Esau na akamwambia aende mwituni alete nyama na amtengenezee chakula. Akamwambia kwamba baada ya chakula atampa baraka za Mungu.


Rebeka alikuwa nje ya hema ya Isaka. Akasikiliza alichosema Isaka. Rebeka alitaka Yakobo apate hizo baraka vile Mungu alivyoahidi. Kwa haraka Rebeka alimwita Yakobo. Alimwambia aende amletee wana mbuzi wawili. Rebeka alitengeneza kitoweo kizuri cha kuvutia kutoka kwa hao mbuzi.

Akashona ngozi za wale wana mbuzi juu ya mikono, viganja na shingo ya Yakobo ili awe na malaika mwilini kama Esau. Tena Yakobo akavaa nguo za Esau na kujifanya Esau.

Mungu alikuwa amesema kwamba Yakobo atapata baraka. Mungu huwa anatimiza ahadi zake. Rebeka alifadhaika aliposikia Isaka akisema kwamba atampa Esau baraka. Alimtuma Yakobo amdanganye Isaka. Angeamini Mungu bila kudanganya.

Yakobo alimpelekea Isaka chakula, alikuwa anatetemeka. Baba yake atajua kwamba yeye si Esau? Akamuita, “Babangu.” “Ni nani?” Isaka aliuliza. Yakobo alijibu, “Mimi Esau, mwanao mkubwa. Nimepata mawindo uliyotaka. Amka ukae na ule chakula chenye nimetengeza.”

Isaka alishuku na akauliza, “Umepataje upesi hivyo?” “Mungu alinisaidia kupata.” Yakobo alijibu. Isaka alijanganyikiwa. Kwa sauti ni Sauti ya Yakobo. Polepole alinyosha mikono yake. “Karibia hapa nami nitakupapasa ili nijue kama wewe ni mwanangu Esau.” Isaka alimpapasa mikono yake ya malaika na kufahamu kwamba ni Esau. Akasema, “Kweli ni Esau.” Akala hicho chakula.



Yakobo alimsongea Isaka. Isaka aliponuzia harufu ya kondeni kwa nguo za Esau na alikubali kwamba ni Esau. Kwa hivyo akambariki Yakobo na kumfanya mrithi wa ahadi za Mungu.

Bunde si bunde Esau alifika na mawindo ya Isaka. Isaka alikasirika sana akauliza, “Nimebariki nani?” Isaka alijua alikuwa Yakobo. Isaka alimwambia kwamba Yakobo alimuletea chakula akakula na kumbariki. Esau alipiga magoti akimsihi Isaka ambariki pia. Lakini haingewezekana Esau apate kwa sababu alikuwa amembariki Yakobo.

Mungu alikuwa amesema kwamba Yakobo atapata baraka. Lakini Yakobo alipata baraka kwa wivu na udanganyivu na hii haimpendezi Mungu. Maneno ya Mungu yalitimizwa lakini kwa ajili ya Rebeka na Yakobo kutumia uongo, uliokuwa na huzuni pia. Esau alikasirikia Yakobo. Alimchukia na akapanga kumua. Yakobo alitoroka kutoka nyumbani. Rebeka hakuendelea kumuona mwanawe mpendwa Yakobo. Kwa miaka mingi Yakobo aliishi mbali na nyumbani kwao.